# HALMASHAURI YA WILAYA BAHI

*Simu:* *+255 26 2961400*
*Nukushi.:* *+255 26 2961401*
*Barua pepe:* *info@bahidc.go.tz*
*ded@bahidc.go.tz*
*Tovuti:* *www.bahidc.go.tz*

*Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji,*
*S. L. P. 2993,*
*DODOMA,*
*TANZANIA.*

## TAARIFA KWA UMMA

### KUHUSU MGOGORO WA ARDHI KATIKA KIJIJI CHA MAKANDA KILICHOPO WILAYA YA BAHI

Mnamo tarehe **30 Agosti, 2017** Gazeti la *Raia Mwema* **Toleo Na. 525 (ISSN 1821-6250)** liliandika habari yenye kichwa cha habari kilichosomeka ***"MGOGORO WA ARDHI BAHI WAENDELEA LICHA YA RUGIMBANA KUJITOSA"***. Katika habari hiyo Mwandishi aliandika mambo mengi ikiwa ni pamoja na wataalamu kuwapotosha viongozi yaani Mkuu wa Wilaya ya Bahi, Mhe. Elizabeth Kitundu na Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Mhe. Jordan Rugimbana, na kwamba mgogoro huo unaendelea kutokana na baadhi ya viongozi kulifanyia biashara eneo hilo ingawa viongozi hao hawakutajwa bayana kuwa ni akina nani.

Mwandishi alieleza kuwa mgogoro huo ulianza baada ya eneo la takriban hekta 1,000 lililotengwa kwa ajili ya malisho ya mifugo, hifadhi ya misitu na vyanzo vya maji kuvamiwa na kufanyiwa shughuli tofauti na zilizokusudiwa. Wilaya inasikitishwa na habari hiyo ambayo kimsingi imeegemea upande mmoja kwani wataalamu waliofanya kazi hiyo wamelaumiwa bila kupewa nafasi ya kueleza hali halisi ya mgogoro huo.



Scanned by CamScanner

Kwanza mgogoro huu ulileta na wafugaji mwaka 2016 ambapo Mkuu wa Wilaya alituma Wataalamu wa Ardhi, Maliasili, Mazingira, Kilimo na Mifugo kwenda kushauri namna ya kumaliza mgogoro huo. Wataalamu hao walienda tarehe 25 hadi 28 Oktoba, 2016 na kukutana na wananchi mbalimbali, Serikali ya Kijiji pamoja na walalamikaji ili kuona eneo husika linalolalamikiwa.

Baada ya Wataalam hao kufika Makanda hakuna aliyekuwa na uhakika wa eneo linalolalamikiwa kwa maana ya kujua mipaka yake na ukubwa wake. Wahusika waliposhindwa kuonesha eneo husika ilibidi watafutwe wananchi waliokuwepo wakati huo na kuwapeleka wataalam katika eneo walilodai kuwa lina mgogoro. Hata hivyo, walionyesha alama za rangi nyekundu na nyeupe zilizopakwa kwenye mibuyu wakidai kuwa ndiyo mipaka ya eneo husika.

Wataalamu walichukua jira (coordinates) na kuziweka kwenye ramani ambapo walishindwa kuchora kwa kuwa hazikuwa na umbo bali zilikuwa zimesambaa. Baadae wataalam waliwataka walalamikaji waoneshe eneo hilo ambapo nao hawakuweza. Wataalamu walienda mbali na kutafuta hiyo amri halali kama imetaja ukubwa wa eneo hilo na mipaka yake na walielezwa kuwa hakukuwa na amri ya maandishi ila Mkuu wa Wilaya wakati huo alitoa tu tamko kwenye Mkutano wa hadhara uliofanyika tarehe 25/07/2010 na kutaka eneo hilo liheshimiwe.

Wataalam walishindwa kufanya kazi kwani hakukuwa na kumbukumbu ya eneo hilo kimipaka hivyo, haikuweza kubainika nani amevamia na wapi amevamia. Hata Serikali ya Kijiji ilikiri kuwa mwaka 2010 kulikuwa na eneo ambalo walitaka kuwaondoa wakulima wa jamii ya kisukuma kwa kutumia kigezo cha kutenga eneo hilo kama la hifadhi ya misitu, vyanzo vya maji na malisho.



Scanned by CamScanner

Baada ya kuona hali hiyo wataalam walishauri kuwa haiwezekani kulinda eneo hilo bila kulitenga kisheria na hivyo walishauri uandaliwe Mpango wa Matumizi ya Ardhi wa Kijiji cha Makanda ambao utasimamiwa kisheria na eneo litajulikana wazi na mipaka yake kubainishwa kisheria.

**Kuhusu kuandaa Mpango bila kuwaondoa wavamizi kama ilivyodaiwa kwenye habari hiyo**, ilitokana na kutokuwa na mipaka iliyobayana na eneo hilo kutengwa bila kuzingatia sheria. Hii inathibitishwa na ukweli kwamba eneo moja haliwezi kutengwa kwa matumizi ya jumla ya Hifadhi ya Msitu, Hifadhi ya vyanzo vya maji na malisho bila kubainishwa mipaka ya kila matumizi kwani haya ni matumizi yasiyoshabihiana.

Kwa mujibu wa kifungu cha 18 (1) (a) cha Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Mwaka 2007, Mamlaka ya upangaji wa matumizi ya ardhi ya kijiji ni Serikali ya Kijiji husika na hutakiwa kuwepo kwa mihtasari husika kitu ambacho hakikufanyika hivyo kukosa nguvu ya kisheria.

Ukiangalia maelezo ya mlalamikaji yanaonyesha kuwa eneo hilo ambalo wanaita Mbuga ya Chibululu ilitengwa kwa Matumizi ya vijiji sita vya Bankolo, Mkakatika, Uhelela, Makanda, Chonde na Lamaiti kitu ambacho hakikufuata utaratibu kwani Kifungu 13 cha Sheria ya Ardhi ya Vijiji namba 5 ya mwaka 1999 jambo hilo hufanyika kukiwepo makubaliano na hakuna makubaliano yoyote ya kimaandishi kati ya vijiji hivyo.

Katika Mkutano Mkuu wa mwezi Julai 2014 wananchi wa Makanda waliomba kubadilisha Matumizi ya eneo hilo wakidai kuwa eneo la Bankolo limeshatumiwa kwa kilimo na hakuna malalamiko yoyote toka kijiji cha Bankolo na Amri wanayoisema haikutaja kijiji cha Bankolo.



Scanned by CamScanner

- **Kuna hoja kuwa Mkuu wa Mkoa alisema kuwa wavamizi wote watoke ndio kazi ya Uandaaji wa Mpango ianze.** Hii si kweli kwani Mkuu wa Mkoa alifika kijijini Makanda tarehe 12/01/2017 wakati Wilaya ilishapanga kuanza kazi hiyo tarehe 13/01/2017 na akaelekeza kuwa kazi hiyo ifanyike ili kubaini ukweli na atatuma Mtaalamu toka Mkoani ili ashiriki zoezi hilo na alituma kama alivyoahidi.

Aidha, **ipo hoja kuwa baadhi ya wavamizi waliingizwa kwenye kamati ya uandaaji wa Mpango wa Matumizi ya Ardhi**. Kwa Mujibu wa Sheria na miongozo ya Uandaaji wa Matumizi ya Ardhi wajumbe wa Kamati ya Matumizi ya ardhi hutokana na Makundi ya watumiaji wa ardhi kulingana na vitongoji na kuzingatia suala la jinsia.

Wajumbe husika wanapendekezwa na Serikali ya Kijiji na kupitishwa na Mkutano Mkuu na kwa mgogoro huo wafugaji walipewa nafasi walete mapendekezo yao na kati ya majina 5 majina 3 yalipitishwa kwenye Mkutano Mkuu wa Kijiji cha Makanda kilichoketi tarehe 13 Januari 2017 ambapo majina hayo yalisomwa na kupitishwa hivyo sheria ilizingatiwa. Wajumbe wote wa Serikali ya Kijiji huingia kwa vyeo vyao kwakuwa wao ndio wapangaji wa Mpango kwa mujibu wa Sheria hivyo huwezi kuwaacha.

Wataalamu tunawaheshimu sana viongozi wetu na tunatekeleza kwa wakati maagizo mbalimbali wanayoyatoa. Pia, tunawaheshimu wananchi wote kwa makundi yao kwa kuwasaidia kutatua kero zao kwa wakati kwani tunafanya kazi kwa weledi na kwa kutumia sheria zilizopo bila kushinikizwa na upande wowote. Kwa mujibu wa habari hiyo eneo linalotajwa kuwa na mgogoro ni takribani hekta 1,000 ambapo ni sawa na ekari 2,470.



Scanned by CamScanner

- Ukweli ni kuwa kupitia Serikali ya Kijiji na Mkutano Mkuu wa Kijiji wa tarehe 23 Januari 2017 limetengwa eneo lenye ukubwa wa ekari 4,219.2 sawa na hekta 1,708.2 kwa ajili ya malisho ya mifugo. Hivyo, hakuna sababu za msingi za kuendelea na malalamiko.

Ukichunguza kwa undani mgogoro huu unazushwa kwa maslahi ya watu binafsi ya kisiasa ili kuwachanganya wananchi, wataalamu na viongozi kwani kwa upande wa wananchi mgogoro huo hauna faida na waliridhika na utaratibu uliofanyika.

Wataalam wanashauri kuwa walalamikaji wafuate taratibu za kisheria kutoa malalamiko yao ambapo kifungu cha 58 cha Sheria ya Matumizi ya Ardhi kinaeleza kuwa mtu yeyote anayeona hajaridhika na uandaaji wa Matumizi ya Ardhi anatakiwa kukata rufaa kwenye Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya au Mahakama Kuu iliyo na Mamlaka katika eneo linalolalamikiwa. Hivyo, Mpango wa Matumizi ya Ardhi wa Kijiji cha Makanda ulishaandaliwa na kupitishwa na Mkutano Mkuu wa kijiji hicho wa tarehe 23 Januari, 2017 (muhtasari upo) kwa Mujibu wa Sheria mwenye malalamiko yake afuate utaratibu uliowekwa kisheria.

Imetolewa na,

Benton J. Nollo

**Mkuu wa Kitengo cha Teknolojia, Habari,**

**Mawasiliano na Mahusiano (W)**

**BAHI**



Scanned by CamScanner